


OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE

Simu: 028-2227148

Fax: 028-2227140

E-mail: ded.karagwe@kagera.go.tz,



S. L. P. 20,

KARAGWE

TANGAZO KWA VYOMBO VYA HABARI NA UMMA KWA UJUMLA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, anapenda kuwatangazia wafugaji wote wa **ng'ombe** Wilayani Karagwe, kuwa kutakuwepo na chanjo ya ugonjwa wa **Miguu na Midomo – SUNNA** (Feet and Mouth Disease (FMD)) kwa gharama ya shilingi **Elfu Tatu (Tsh.3,000/=)** kwa kila ng'ombe na itakayofanyika kwa awamu **tano** kama ifuatavyo;

- i) Kuanzia tarehe **09/04/2018** hadi **20/04/2018** chanjo itafanyika kwa Kata za **Rugera, Kihanga, Ndama, Chanika, Kituntu, Kanoni na Igurwa;**
- ii) Tarehe **23/04/2018** hadi **30/04/2018**, chanjo itafanyika kata za **Kayanga, Bugene, Nyakahanga, Ihanda na Chonyonyo;**
- iii) Tarehe **01/05/2018** hadi **10/05/2018** chanjo itafanyika Kata za **Kamagambo, Kiruruma, Nyabiyonza, Bweranyange na Kibondo;**
- iv) Tarehe **11/05/2018** hadi **25/05/2018** chanjo itafanyika Kata za **Nyaishozi, Nyakabanga, Nyakakika, Ihembe na Rugu na**

- v) Tarehe **28/05/2018** hadi **08/06/2018** Chanjo itafanyika katika **Vitalu/Blocks** zote zilizopo wilayani Karagwe.

Aidha chanjo hii ni ya lazima na hatua kali zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria dhidi ya yeyote atakayekaidi agizo hili. Na kuanzia sasa ni marufuku kwa mfugaji yeyote kuchanja ugonjwa wowote wa mlipuko pasipo idhini ya Halmashauri.

Limetolewa mnamo tarehe 30/03/2018 na;



GODWIN M. KITONKA,
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
KARAGWE.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE